# Learning by Ear 2012 – Corruption – The Elephant in the Room

## Episode 09 – "Votes: Not for Sale"

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

- NARRATOR

Scene 1:

- Jeffrey (MALE, 58)
- Sylvia (FEMALE, 19)
- Crowd (min 5 persons, male and female mixed)
- Voter (FEMALE, 45)

Scene 2:

- Alfayo (MALE, 58)
- Jennifer (FEMALE, 53)
- Lydia (FEMALE, 16)
- Helen Drayson (FEMALE 30's)

**<u>Intro:</u>**

**0. Narrator:** Hujambo na karibu kusikiliza sehemu ya tisa katika mfululizo wa Vipindi vya “**Noa Bongo Jenga Maisha yako**” katika mchezo huu wa redio kuhusu ufisadi, kwa jina “**Tembo Nyumbani**”, ambapo tunapokaribia kufika kilele cha hadithi hii kuhusu maisha ya familia ya Bwana Odhiambo na rafiki yake, Jeffrey. Katika kipindi kilichotangulia, Alfayo Odhiambo, anakiri mbele ya mkewe, Jennifer Odhiambo, kwamba kampuni yake inahusika moja kwa moja na sakata ya nishati, ambayo pia inawahusu mawaziri, huku binti yao Lydia na rafiki yake Tekla wakifichua kwa vyombo wa habari kuhusu kashfa ya ulaji rushwa shuleni .

Na katika kipindi cha leo chini ya Kichwa “ **Kura: haziuzwi**” Familia ya Odhiambo inajiandaa kumkabili baba yao, huku Jeffrey akiwa katika

mkondo wake wa dakika za mwisho mwisho

kufanya kampeni kabla ya uchaguzi mkuu.

## Scene One:

**1. Atmo:** **Outside Atmo,Music playing. crowds gathered for political rally**

**2. Jeffrey:** **(shouting**) Pesa zao chukueni lakini kura msiwapigie .. tumeelewana - Zawadi mpokee lakini kura msiwape ... sawa!

**3. Crowd:** **(chanting)** Pokeeni pesa zao lakini kura msiwapigie!

**4. Jeffrey:** **(to rounds of applause)** Asanteni sana kwa kufika kwenu hapa. Sitaki kuchukua muda wenu mwingi. Kama wengi wenu mnavyofahamu, hapa nchini kwetu, ufisadi umekithiri na kuwa jambo la kawaida. Ni sawa na mripuko wa maradhi, hali

inayozorotesha uchumi na maendeleo ya taifa letu. Na hii ndio sababu niko hapa leo!

**5. Crowd:** **(cheers and applause)**

**6. Jeffrey:** Sisemi kwamba nitabadilisha mambo kwa usiku mmoja. Na wala sitatoa ahadi za uongo. Lakini ninachowasihi, ni kwamba mnipigie kura na niaahidi kuwatumikia bila kuchoka, kuona kwamba tunaangamiza magonjwa na ufisadi.

**7. Crowd:** **(cheers)**

**8. Jeffrey:** Mabadiliko haya hayatatokea mara moja. Huenda yatachukua muda. Lakini mkinipigia kura, naahidi tutaweka mikakati ya kuendeleza taifa letu kiuchumi na kimaendeleo, kujenga taifa lenye uwazi na uaminifu kwa manufaa ya kila mmoja wetu. Pesa mpokee kutoka kwa wapinzani wangu

waliojaza magunia ili kuja kuwahonga- sawa lakini msithubutu kuwapigia kura. Kwa kwasababu nia yao sio kuangamiza ufisadi.- bali kuikuza. Asanteni sana!

**9. Crowd:** **(big cheers)**

**10. Sylvia:** Pongezi sana, Jeffrey! Huo ni ujumbe mzito sana ambao naamini umepokelewa vizuri. Yaani umegonga ndipo... Hebu tazama kule, lile kundi la John Maina likigawa pesa kwa wapiga kura. Lakini watu hawaonekani wakichangamkia pesa hizo.

**11. Jeffrey:** Ni kweli. Wacha tuombe tu kwamba kauli mbiu yetu itakita mizizi. ...Lilikuwa wazo la busara sana Lydia. Lakini wazo hili limekukujia vipi?

**12. Sylvia:** Kwa hakika, eti kuwaambia watu wasichukue pesa, wakati pesa hizo zikiendelea kutolewa

upande mwengine haitoshi..! Sio wengi watakusikiliza hasa wale walio na mahitaji makubwa ya pesa. Hivyo, nikaona bora kuwaambia, ni sawa....wakiwapa pesa hizo wapokee lakini katu wasikubali kuwapigia kura . Kura zao watupigie sisi. Hakuna ajuaye pengine kesho huenda mambo yakabadilika. Na kweli watu wemependa sana semi hiyo.

**13. Jeffrey:** Ndio.... Bila shaka wamekubaliana nasi.

***KW begin***

**14. Voter:** Samahani mheshimiwa. Nimesoma tu kwenye magazeti kuhusu sakata hili la ulaji rushwa shuleni- Je, unafahamu jinsi walimu wanavyopokea rushwa. Nakushukuru sana kwa kufichua kashfa hiyo. Pia, uovu huu umekuwa ukiendelea shuleni

wanakosomea watoto wangu. Mimi nina watoto saba na sina pesa za kuwahonga walimu ili watoto wangu waweze kupata matokeo bora.

**15. Jeffrey:** Binti, nafurahi kwamba unaunga mkono juhudi hizi. Baada ya kufichua kashfa hii, kitakachofuata sasa ni kuunda sheria madhubuti za kukabiliana na ufisadi. Walimu wenye tabia ya kupokea rushwa lazima wafutwe kazi. Lakini tunapaswa kwenda hatua kwa hatua. Hapana shaka hili ni suala nitakalolipa kipaumbele wakati nitakapoingia bungeni.

**16. Voter:** Sawa kabisa, bila shaka mimi na familia yangu tutakupigia kura. Lakini kwanza wacha nirudi kule ambako pesa zinatolewa na wapinzani wako ili angalau niweze kupata sehemu yangu – Naweza kununua chakula cha jioni kwa ajili ya familia yangu.

**17. Jeffrey:** Nashukuru sana kwa kufika kwenu.

***KW end***

**18. Sylvia:** Jeffrey. Kabla hujaondoka hebu tazama anayekuja. Ni John Maina, waziri wa nishati mwenyewe. Yuaonekana hana furaha.

**19. Jeffrey:** Mimi siwezi kumtoroka. Kama ana jambo la kusema aje namsuburi hapa, mimi simuogopi.

**20. Maina:** **(Maina shoves Jeffrey to the ground and kicks him)**

Ondoka hapa, Thiongo hili ni eneo langu.

**21. Jeffrey:** **(groaning in pain)** Owwww…

**22. Maina:** Hawa ni wafuasi wangu kwasababu tunawaangalia vizuri. Unawaambia nini? Kwamba eti utakomesha ufisadi? Wenyewe wanafahamu kwamba wakinipigia kura hawatakosa chakula cha kila siku.

**23. Jeffrey:** **(getting up again)** Ni kwa sababu hawafahamu kwamba kwa kukupigia kura wewe ni kukusaidia kujaza tumbo na akaunti zako za benki. Maina, ni kweli hawa watu ni maskini, lakini si wajinga. Wanaweza kutofautishamMtu mlaghai na mwenye nia nzuri. Na hivi karibuni watakuja kutambua wewe ni mtu wa aina gani. Twende Sylvia.

**24. Maina:** Tayari umeonywa Jeffrey. Watu wanaojaribu kunipinga wanahatarisha maisha yao. Na wataishia kaburini. Kama unataka kupambana na mimi kumbuka mimi si mtu wa kusahau haraka.

**25. Jeffrey:** Cha msingi Bwana Maina ni ufahamu kwamba muda wako wa kuendelea kuwa mamlakani umekwisha! Na utakuja kujuta.. Ingelikuwa mimi, sasa ningeanza kutayarisha vyeti vyangu na kutafuta kazi mahali kwengineko. Subiri tu utaona.. siku zako zimekwisha.

**End of Scene One**

**26. Narrator:** Jeffrey sasa ameanza kupata maadui wa kisiasa. Na maisha yake huenda yamo hatarini zaidi. Bado anapiga moyo konde licha ya hatari iliyopo dhidi ya maisha yake katika juhudi za kubadilisha mambo nchini mwake hasa kuangamiza ufisadi. Alfayo Odhiam pia yuko katika mkondo huo huo wa kuhatarisha maisha. Kwa ushirikiano na Jeffrey, ameamua kusaidia kufichua kashfa kubwa katika sekta ya nishati ambayo yeye mwenyewe anahusika.

## Scene Two:

**26.a SFX** phone rings

**26.b Jennifer:** Jennifer Odhiambo

**26.c Sylvia:** (On phone) Habari mama, ni mimi Sylvia. Haujambo?

**26.d Jennifer:** Mimi ni mzima, Nafurahi kusikia sauti yako. Lakini tunawasiwasi kiasi inapokaribia siku ya uchaguzi.

**26.e Sylvia:** Hiyo ndio sababu ya kukupigia simu hii. Tumemtuma mtu mmoja kutoka ofisini kwetu ili kuzungumza nanyi kuhusu suala hili. Jina lake ni Helen. Unaweza kumuamini. Samahani, nina haraka, bado tuko katika kampeni. Tutaonana baadae mama. (**Hangs up**)

**26.f Jennifer:** Subiri: **(sighs) (To Alfayo)** Huyo alikuwa ni binti yetu. Wanamtuma mtu kuja kuzungumza nasi kuhusiana na masuala ya usalama.

**27. Alfayo:** Nahisi ni kama mnyama aliyefungiwa kibandani, Jennifer (….) Kufungiwa nyumbani nisiweze

kutoka nje. Je hiki ni kionjo tu? Au tutaishia kufungwa gerezani maisha?

**28. Jennifer:** Naomba isiwe hivyo. Naomba liwe kama wingu linalopita tu na kwamba mambo haya yatakuja kupita na kusahaulika kabisa ili turejee maisha yetu ya kawaida.

**28a. SFX:** **Knock at door**

**29. Helen:** Habari za leo. Kama sijakosea wewe ni Bibi na Bwana Odhiambo. Jina langu ni Helen Dryson kutoka shirika la "**Komesha Ufisadi sasa**". Amenituma kuja kuwasaidia hasa wakati huu mgumu. Je, mnaweza kunipa muda wenu?

**29a. SFX** **Door opens, Footsteps enter, door closes**

**30. Alfayo:** Bila shaka, Helen, karibu ndani.

**31. Helen:** Asanteni sana. Ninataka kuzungumzia mambo machache ambayo ni muhimu sana. Bw. Odhiambo unakumbuka umetoa taarifa yako ya ushahidi kwa shirika la **Komesha Ufisadi sasa**, na tuko katika harakati za kuandaa ripoti kamili ambayo itatolewa kwa vyombo vya habari leo jioni.

**32. Jennifer:** Leo Jioni...alaah!

**33. Helen:** Ndio, lakini usiwe na wasi wasi, hakuna haja ya kuwa na hofu kabisa. Punde tu sakata hili litakapo wekwa wazi kwa umma, ndipo itakuwa rahisi kushughulikia suala hili. Ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, usizungumze moja kwa moja na vyombo vya habari, bila ya kauli kutoka kwetu. Kila kitu unachozungumza lazima kipitie ofisi yetu. Ni muhimu sana.

**34. Alfayo:** Kwanini iwe hivyo?

**35. Helen:** Kwa sababu baadhi ya waandishi wa habari ni vibaraka wa waziri wa nishati. Wanalipwa kudumisha jina zuri la wizara husika. Kwa namna hiyo, wanaweza kubadilisha taarifa yako, au kukuelewa vibaya hivyo kutoa taarifa za uongo. Hali hii inaweza kukuweka mashakani na lazima tuwe waangalifu kwasababu kampuni yako

inahusika katika kashfa hii. Kwa hiyo, usiwe mtu wa kupayuka.. Sawa?

**36. Alfayo:** Hiyo ni sawa, kumbe. Unadhani mambo yanaweza kugeuka na kuwa mabaya zaidi?

**37. Helen:** Lazima tujiandae kwa chochote. Mara nyingi watu wanaopuliza kipenga kwa kashfa kama hizi huwa mashakani sana – kumbuka, sio tu umefichua kashfa hii ya nishati bali pia kuwaweka familia, watu na kabila lako mashakani.

**38. Alfayo:** Lakini hili si suala la kabila langu. Ni Ufisadi, na jinsi watu wanavyotumia mamlaka yao vibaya kujinufaisha kifedha.

**39. Helen:** Nakubaliana nawe, na natumai kwamba watu wataelewa yote unayosema. Lakini nakutahadharisha, wakati taarifa hii itakapotolewa

kwenye vyombo vya habari baadhi ya watu wataanza kukuepuka.

**40. SFX:** **knock at the door, door bursts open**

**41. Lydia:** Ahh, Baba, kumbe uko hapa! Kuna tatizo lolote?

**42. Alfayo:** Habari gani Lydia. Helen hapa anajaribu kunieleza mambo fulani. Anafanya kazi katika shirika la Jeffrey.

**43. Helen:** Nimekuwa nikijaribu kumtahadharisha babako asiwe mtu wa kuzungumza sana na kwamba mtu yeyote kutoka familia hii asizungumze na vyombo vya habari bila ya kwanza kuwasiliana nasi. Sakata hili ya nishati litakuwa kwenye magazeti kesho. Kwa hivyo, bila shaka itazua taharuki kubwa sana.

**44. Lydia:** Sasa basi kwanini usibakia nyumbani, Baba? kesho mimi, Isaac na Sylvia tutakuwa viwanjani kumpigia kampeni Jeffrey, lakini wewe unaweza kujificha hapa nyumbani tu kisha baadaye kwenda kwenye mgahawa ambako Jeffrey na kundi lake watakuwa wakisubiri matokeo?

**45. Alfayo:** Wazo zuri sana hilo Lydia. Tunaweza kufuatilia matokeo ya uchaguzi pamoja. Pita ndani. Kwa hivyo, Helen leo tutabaki hapa nyumbani na kesho jioni tutakuwa mgahawani kufuatilia matokeo hayo. Si hivyo ni sawa?

**46. Helen:** Hiyo ni sawa kabisa. Hapa nyumbani utakuwa na usalama wa kutosha leo na kesho. Lakini nakusihi usiondoke kwenda mahali kwengine. Na wewe, Lydia: najua siwezi kukuzuia wewe na kakako kwenda kumpigia kampeni Jeffrey, lakini tafadhali muwe waangalifu sana.

Tayari Jeffrey ameanza kupata vitisho vya kuuawa. Mimi naondoka sasa, lakini unaweza kunipigia simu wakati wowote ukihitaji msaada wangu. Kila la kheri.

**47. Alfayo:** Sawa Heleni, nashukuru kwa mawaidha yako. Ukituhitaji unajua wapi kwa kutupata.

**48. Jennifer:** Naomba mambo haya yamalizike. Ni kama tuko kifungo cha nyumbani. Kwani tumefanya nini kuingia katika balaa hili lote?

**End of Scene Two**

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**49. Narrator:** Na hadi hapo msikilizaji tunafika mwisho wa sehemu hii ya tisa kwenye mfululizo wa mchezo wa redio kuhusu Ufisadi kwa Jina "**Tembo Nyumban**i" hadithi inayosimulia hali halisi ya maisha. Je, maisha yatakuwaje kwa familia ya Odhiambo wakati sakata la nishati litakapowekwa hadharani kupitia vyombo vya habari? Ni nini kitakachotokea siku ya uchaguzi? Je, Jeffrey atafaulu kuingia bungeni? Watu watamuanini na kumpigia kura kwa kuzingatia sera zake za kumaliza ufisadi?

Hayo yote ni katika sehemu ya kumi na ya mwisho ya mchezo huu. Ukipenda kusikiliza tena makala haya, unaweza kutembelea mtandao wetu dw.de/lbe. Au ukiwa na maoni pia usisite kututumia kupitia ukurasa wetu wa Facebook. Asante kwa kutusikiliza hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!